Nuru ya Kiswahili, Juzuu 5(1), Juni 2026:146-172
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru51.146172

# Usawiri wa Utandawazi katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili: Mifano kutoka *Babu Alipofufuka* (2001) na *Makuadi wa Soko Huria* (2002)

**Bakita Malindi**
**Mhadhiri Msaidizi, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**
bakitafocus@gmail.com

**Anna Kyamba**
**Mhadhiri, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**
anna.kyamba@out.ac.tz

**na**

**Mohamed Maguo**
**Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**
mohamed.omary@out.ac.tz

## Ikisiri

Makala hii inalenga kubainisha vipengele mbalimbali vya utandawazi vinavyojitokeza katika riwaya za kisasa za Kiswahili. Riwaya teule zilizotumika wakati wa ukusanyaji wa data na uchanganuzi wake ni *Babu Alipofufuka* (2001) na *Makuadi wa Soko Huria* (2002). Riwaya hizi zimeteuliwa kwa kuwa ziliandikwa kati ya mwaka 2000 hadi 2010 kipindi ambacho utandawazi ulizungumziwa na wanazuoni wengi katika fasihi ya Kiswahili na hata nje ya fasihi. Pia, riwaya teule zinaakisi vizuri hali halisi ya utandawazi nchini Tanzania. Data za makala hii zilipatikana kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa matini katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili. Aidha, data zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli, ambapo maelezo yalitumika kuwasilisha uchambuzi wa data. Nadharia ya Uhalisia imetumika katika uchambuzi wa data na uwasilishaji wake. Utafiti ulibaini vipengele mbalimbali vya utandawazi vilivyojitokeza katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili ambavyo ni: kushamiri kwa uwekezaji, umilikishwaji wa ardhi, kushamiri kwa ubinafsishaji, kuingizwa kwa utamaduni wa kigeni na ukwepaji wa kodi. Aidha, tunapendekeza tafiti nyingine zifanyike kuhusu ulinganisho kifani au kimaudhui

katika riwaya za kisasa za Kiswahili na riwaya zilizoandikwa kabla ya utandawazi.

**Maneno muhimu**: Utandawazi na riwaya za kisasa

## Utangulizi

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kiubunifu ili kueleza tajiriba mbalimbali za maisha ya mwanajamii (Msokile, 1993). Nao Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa fasihi inawasilisha hali, maingiliano, mivutano na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira yake. Fasihi hupokea mabadiliko kulingana na maendeleo ya jamii husika. Senkoro (2007) anasema kuwa fasihi hubadilika kulingana na mabadiliko ya jamii. Mabadiliko hayo ndiyo husababisha kuibuka kwa namna mpya ya utunzi wa tanzu mbalimbali za fasihi kama vile tamthiliya, ushairi na riwaya. Mabadiliko haya yametokana na utandawazi uliochangia kuwapo kwa mwingiliano wa kijamii pamoja na masuala ya elimu.

Thomas (2005) anasema kuwa utandawazi ni mchakato unaopanua mahusiano ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kuvuka mipaka ya kitaifa na kufanya mataifa kuwa sehemu ya mfumo mmoja wa kimataifa. Mfumo huo unahusisha mtiririko wa bidhaa, huduma, mitaji, taarifa, teknolojia, watu na tamaduni kwa kasi kubwa. Kwa mtazamo huu, maendeleo yanayotokea katika taifa moja yanaweza kuwa na athari kwa mataifa mengine. Hata hivyo, ni wazi kuwa vipengele vya utandawazi tulivyovibainisha vilikuwepo tangu awali, ila kwa sasa vimechukua sura mpya kutokana na jamii kukua na kuendelea katika zama hizi za utandawazi. Thomas (2005) anataja sifa kadhaa za utandawazi: Mosi, kuunganisha dunia kupitia teknolojia za habari na mawasiliano. Pili, unahusisha uhuru mkubwa wa biashara na uwekezaji wa kimataifa kupitia sera za uchumi huria. Tatu,

huchochea usambazaji wa maarifa, ubunifu na teknolojia kati ya mataifa. Nne, unaongeza mwingiliano wa tamaduni, ambapo watu hukutana na kubadilishana mitazamo na kuathiriana katika lugha, mavazi, muziki na mitindo ya maisha. Tano, huimarisha ushirikiano wa kimataifa katika kushughulikia changamoto zinazovuka mipaka kama vile magonjwa ya mlipuko na ugaidi. Kimsingi, katika ulimwengu wa sasa utandawazi umebadilisha namna watu, taasisi na mataifa yanavyoshirikiana, huku ukizalisha fursa na changamoto zinazohitaji ufumbuzi. Utandawazi ni miongoni mwa masuala ambayo yamekuwa yakisawiriwa katika fasihi ya Kiswahili, ikiwamo riwaya.

Riwaya ni mojawapo ya fasihi ambayo husawiri maudhui mbalimbali yanayoenda sambamba na mabadiliko ya jamii husika. Maelezo haya yanashadidiwa na Kezilahabi (2006) kwa kueleza kuwa utanzu wa riwaya ni legelege na tepetepe, wenye kugeukageuka na kubadilika kulingana na mabadiliko ya kijamii. Masimo (2023) anaongezea kuwa, uandishi wa riwaya ulikuwa unapokea mabadiliko kadiri muda ulivyosonga mbele. Kwa mfano baadhi ya riwaya zilizoandikwa kuanzia miaka ya 1990 na kuendelea zimebeba sura mpya ya kiutandawazi inayozitofautisha na riwaya za mwanzo zilizokuwa na sifa ya kutumia lugha yenye maadili na iliyobeba maudhui ambayo yalisawiri hali halisi ya maisha ya jamii ya wakati huo. Kimsingi, mabadiliko hayo ndiyo hufanya kukawa na aina tofauti za riwaya kama vile riwaya za kisasa. Naye, Selemani (2012) anaeleza kuwa riwaya za kisasa ni zile zenye maudhui mapya yanayosawiri hali ya ulimwengu wa sasa[1] inayohusisha mabadiliko ya kijamii, elimu na tamaduni kama vile

[1] Selemani (2012) ulimwengu wa sasa ni dunia ya wakati huu, yenye maendeleo, mabadiliko, changamoto na fursa zinazotokana na mazingira ya kisasa.

masuala ya uvutaji bangi na madawa ya kulevya, ugaidi, ndoa za jinsia moja na biashara haramu.

Tangu utandawazi ulipoanza kuzungumziwa katika fasihi ya Kiswahili, wamejitokeza watafiti mbalimbali waliochunguza uhusiano wa utandawazi na fasihi ya Kiswahili, ikiwamo riwaya ya Kiswahili. Miongoni mwao ni Kevogo (2017), Masimo (2023), na Musembi na Simiyu (2024). Mambo yaliyochunguzwa na watafiti hao ni matatizo mbalimbali ya viongozi wa nchi zinazoendelea katika enzi za utandawazi, taathira za utandawazi na manufaa yake katika bara la Afrika na mkengeuko (hali ya tukio moja kuchukua kasi na kulifanya tukio la awali kusahaulika) wa utamaduni wa Waswahili katika riwaya ya Kiswahili zama za utandawazi. Jean (2002) anasema kuwa, mwingiliano wa Wabantu na wageni umechangia kuharibu thamani ya maadili yaliyomo katika jamii ya Wabantu kwa kuthamini mambo mapya yaliyoletwa na wageni. Naye, Oni (2005) anasema kuwa ukoloni, elimu na mwingiliano wa kijamii vimechangia kupotea kwa mfumo wa awali wa mila na utamaduni wetu. Maelezo ya Oni (ktj) yanashadidiwa na Nyonje (2006) na Suakei (2017) kwa kusema kuwa vijana wapo katika hatari ya kupoteza utambulisho kwa kuiga tabia na mienendo ya Kimagharibi ambayo ni tofauti na utamaduni wa jamii ya Kiafrika. Masimo (2023) anajadili zaidi kuwa, familia za Wabantu katika kipindi cha utandawazi zipo katika njia panda za kuacha utamaduni wao na kuthamini mambo ya kigeni yanayoonekana kuwavutia. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa utandawazi umeendelea kuwa miongoni mwa masuala yanayoathiri nyanja mbalimbali za maisha, ikiwamo fasihi. Riwaya kama sehemu ya fasihi huakisi mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni yanayosababishwa na utandawazi. Hivyo, kuna haja ya kuchunguza namna vipengele vya utandawazi vinavyosawiriwa katika

riwaya teule na jinsi vinavyojengwa kisanaa ili kuwasilisha ujumbe kwa jamii.

## Kiunzi cha Nadharia

Makala hii inaongozwa na Nadharia ya Uhalisia ambayo iliasisiwa katika karne ya 19 na Gustav Flaubert na kufafanuliwa zaidi na Goffman mwaka 1952. Wataalamu wengine wanaotoa mchango kuhusiana na nadharia hii ni Lukacs (1979) na Hegel (1971). Naye, Wamitila (2003) anaeleza kuwa, katika hali halisi, riwaya lazima ioneshe hali halisi ya matukio katika jamii husika. Anaendelea kufafanua kuwa thamani ya riwaya ni kuonesha kwa usahihi matukio halisi yanayotokea katika jamii. Hivyo basi, waandishi wa riwaya hawana budi kuusawiri ukweli ulioko katika jamii na kuonesha wazi kila changamoto kwa lengo la kuleta mabadiliko katika jamii. Wamitila (ktj) anabainisha misingi ifuatayo ya Nadharia ya Uhalisia:

(i) Sanaa ionyeshe maudhui ndani ya jamii husika;
(ii) Sanaa iwe na urahisi katika kazi husika;
(iii) Sanaa iwe na uhalisia ambao hubadilika kutokana na mabadiliko ya jamii husika; na
(iv) Sanaa iwakilishe ukweli kwa maneno halisi, iwe aminifu na ioneshe hali halisi ya mazingira.

Utafiti uliozalisha makala hii uliongozwa na msingi wa tatu na wa nne. Misingi hii iliongoza katika kuchambua maudhui ya riwaya teule za kisasa za Kiswahili, yanayoendana na utandawazi kisha kubainisha data zinazohusiana na vipengele vya utandawazi.

## Methodolojia

Katika utafiti uliozalisha makala hii, wango ni riwaya za kisasa za Kiswahili zilizoandikwa kuanzia mwaka 2000 hadi 2010. Tulitumia mbinu

ya usampulishaji lengwa kupata sampuli, yaani riwaya mbili za kisasa za Kiswahili zilizoandikwa kuanzia mwaka 2000 hadi 2010. Riwaya hizo ni *Babu Alipofufuka* (2001) na *Makuadi wa Soko Huria* (2002). Riwaya hizo zimewezesha kukidhi malengo ya makala hii. Data za makala hii zilikusanywa na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa matini, ambapo riwaya teule zilisomwa kwa umakini. Data zilizopatikana zilifafanuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli, ambao hutumia zaidi ufafanuzi wa maelezo katika kuhusisha taarifa mbalimbali za kitafiti.

## Vipengele vya Utandawazi Vinavyojitokeza katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili

Tulibaini vipengele vitano vya utandawazi vinavyojitokeza katika riwaya teule. Vipengele hivyo ni: kushamiri kwa uwekezaji, umilikishwaji wa ardhi, kushamiri kwa ubinafsishaji, kuingizwa kwa utamaduni wa kigeni, na ukwepaji wa kodi. Sehemu zinazofuata zinawasilisha data na mjadala kuhusu vipengele hivyo, kwa kuongozwa na Nadharia ya Uhalisia.

### Kushamiri kwa uwekezaji

Uwekezaji ni kitendo cha kutumia fedha, muda, rasilimali, au juhudi katika jambo fulani kwa lengo la kupata manufaa au faida baadaye (Kalegeya, 2012). Uwekezaji unahusisha mtiririko wa mitaji, teknolojia na biashara. Aghalabu, mtiririko huo huhusisha watu wa kutoka nchi moja kwenda nyingine kwa urahisi kutokana na utandawazi. Naye, Shivji (2006) anaeleza kuwa uwekezaji nchini Tanzania umesababisha matatizo makubwa ya ardhi, kiasi cha watu kukosa maeneo ya kulima, kufuga na makazi. Uwekezaji umesababishwa na ubinafsi wa viongozi wengi na wageni wenye hadhi kutoka nchi za Magharibi kuwadhulumu wananchi haki zao, kama vile uanzishwaji wa miradi mbalimbali, umiliki wa ardhi, na malighafi

zilizozalishwa katika mazingira yanayowazunguka. Kimsingi, uwekezaji ulikuwapo hata kabla ya zama za utandawazi kuenea, ila kwa sasa umepata mabadiliko yanayoendana na hali halisi katika jamii ya sasa. Hata hivyo, uwekezaji ulianza kutumika kwa mapana zaidi na kitaalamu baada ya kuongezeka kwa uchumi wa soko na elimu kipindi cha utandawazi. Uwekezaji katika jamii ya sasa umelenga zaidi kwenye ubinafsi. Kwa muktadha wa utafiti uliozalisha makala hii, uwekezaji umehusishwa na utandawazi kwa sababu utandawazi hurahisisha mtiririko wa mitaji, biashara huru, teknolojia na watu kati ya nchi mbalimbali. Hivyo, wawekezaji wanaweza kuwekeza katika nchi tofauti kwa urahisi zaidi. Hali hii ya kushamiri kwa uwekezaji imedhihirika katika riwaya teule tulizoshughulikia. Hii, kama asemavyo Ntarangwi (2004), inasababishwa na hoja kuwa sanaa huwa na uhalisi ambao huiakisi jamii husika.

Mathalani, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), kushamiri kwa uwekezaji kumejitokeza pale Kiongozi K alipokaa kikao na wageni kutoka Magharibi—akina Dielpiero, Di Livio, Von Heim na Miyazawa—katika ukumbi wa Neo-Casino ili kujadili uwekezaji katika mradi mkubwa wa FKK. Mwandishi anasema:

> **Data Na. 1**
> Macho ya Di Livio na ya K yakatafutana na yalipokutana, Di Livio alianza kwa lafudhi ya lugha yake. “Kuhusu mradi mpya tuliokuwa tukijadiliana uwe upi wiki nzima, mimi naona tuanzishe mradi wa burudani unaoitwa FKK…” (uk. 42)

Dondoo hili linaonesha wageni kutoka nchi za Magharibi walivyokuwa makini katika suala zima la uwekezaji, hadi kutenga muda wao kwa ajili ya kujadili kuhusiana na suala hilo. Katika mjadala huo, walikubaliana kuanzisha mradi wa klabu ya FKK ili kuwaongezea kipato. Suala hili

linadhihirika pale wahusika wageni kutoka nchi za Magharibi na matajiri wachache waliomo nchini wanapojadili miradi kwa maslahi yao binafsi. Lengo kuu la wawekezaji, kama asemavyo Shivji (2006), ni kukuza kipato chao na kujenga utajiri ambao watanufaika nao kwa muda mrefu. Kwa upande mwingine, wananchi wa kawaida hawakuridhika na uanzishwaji wa miradi hiyo kwa sababu walitambua kwamba hawatanufaika nayo.

Katika riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* (2002), suala la uwekezaji limejitokeza kwa namna mbalimbali. Mwandishi anamwonesha Bwana Paul Mooney mwenye asili ya Uingereza, kutaka kuwekeza katika ufugaji wa samaki aina ya kamba huko Rufiji. Pendekezo hili la ufugaji wa samaki lilijadiliwa na watu wa Rufiji, watu wa Dar es Salaam, wanasiasa na watendaji wa wizara. Watu wengi waliohudhuria mjadala huo waliunga mkono suala hilo, isipokuwa wazee na wenyeji wa Rufiji. Mwandishi anasema:

> **Data Na. 2**
> Saa kumi na moja jioni. Ndiyo kwanza mkutano ulioitishwa na Baraza la Mazingira na kufanyika katika Ukumbi wa Utamaduni wa Korea umemalizika. Ulikuwa ni mkutano wa kusikiliza maoni ya wananchi kuhusu mapendekezo ya mwekezaji mmoja wa kutoka Uingereza, Bwana Paul Mooney ambaye alitaka kuanzisha ufugaji wa samaki aina ya kamba katika Delta ya Rufiji (uk. 22).
>
> “Wewe na wenzako mliokuja kutetea huu mradi mmeletwa na mwekezaji. Mmehongwa nyie! Tutaonana tukirudi huko!” Lile kundi pale lilimsakama mwenzao kwa makelele, likasababisha hata makundi mengine kunyamaza na kugeuka kuangalia kilichokuwa kikitokea miongoni mwa hawa watu wa Rufiji (uk. 23).

Nukuu hii inaonesha jinsi Paul Mooney anavyopambana kuwekeza katika ufugaji wa samaki aina ya kamba katika Delta ya mto Rufiji. Zaidi,

tunaoneshwa kuwa, kupitia mkutano ulioitishwa na Baraza la Mazingira, wananchi walionesha kutopendezwa na mwekezaji kutoka nchi za nje kwa sababu walitambua kuwa hawatanufaika kwa chochote, bali watakaoneemeka ni wawekezaji. Maelezo haya yanaendana na ya Dunning (1992) anaposema kuwa lengo kubwa la wawekezaji ni kukuza faida binafsi na ushindani kwa kiwango cha kimataifa, sambamba na kuchochea maendeleo yao kiuchumi. Kupitia msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaosisitiza sanaa iwe na uhalisi ambao hubadilika kutokana na mabadiliko ya jamii husika, tulibaini kuwa mwandishi amefanikiwa kuonesha maisha halisi ya jamii kwa kumtumia mhusika Paul Mooney na wenzake. Wahusika hawa walitumia mbinu mbalimbali za kuwalaghai wenyeji ili wapate nafasi ya kuwekeza katika kiwanda cha samaki. Lupocho aliwasaliti watu wa Rufiji kwa kuunga mkono uanzishwaji wa mradi wa samaki, suala ambalo halikupendwa kabisa na wenyeji wa Rufiji. Baada ya kupokea rushwa kutoka kwa Mooney, Lupocho alisimamia upande wa utetezi wa uanzishwaji wa mradi huo. Wageni kutoka nchi za nje walilazimisha uanzishwaji wa mradi kwa faida zao binafsi. Katika hali halisi, ni dhahiri kuwa kuna baadhi ya wenyeji hupokea rushwa, kisha hutetea wawekezaji na kuwakandamiza wananchi wa kawaida.

Vilevile, kupitia mhusika Alibhai, mwandishi anaonesha kuwa lengo la wageni kutoka nje ya nchi lilikuwa kuwekeza katika miradi mbalimbali. Mwandishi ameyadhihirisha haya kwa kusema:

**Data Na. 3**

Bwana Alibhai alikuwa mmoja kati ya wafanyabiashara kumi wakubwa ambao walihodhi biashara ya nchi za nje, kama muuzaji na mnunuzi wa jumla wa bidhaa. Alikuwa pia na viwanda kadhaa nchini, baadhi yake vya kutengeneza vinywaji baridi na maji ya kunywa. Vingine vya kusindika minofu ya samaki aina ya sangara kule Mwanza na kingine cha Mbagala kilishughulika na samaki

> aina ya kamba, na wakati mwingine pweza na tasi (uk. 117).

Nukuu hii inaonesha jinsi uwekezaji wa viwanda ulivyojitokeza kama kipengele cha utandawazi. Bwana Alibhai, mgeni kutoka nje ya nchi, alipambana katika uwekezaji wa viwanda kadhaa vya kutengeneza vinywaji na vya kusindika samaki. Kupitia msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaosisitiza kuwa sanaa iakisi maisha halisi ya jamii, tulibaini kuwa mwandishi amefanikiwa kuonesha maisha halisi ya jamii kwa kuwatumia wahusika wageni na baadhi ya viongozi waliohimiza uwekezaji mbalimbali kwa kutaka kujinufaisha. Hata hivyo, uhalisi ni kwamba uwekezaji unaojitokeza katika jamii ya sasa unawakandamiza wananchi kwa kuwalaghai kwa mambo madogomadogo na kuwanufaisha wawekezaji binafsi.

**Umilikishwaji wa ardhi**

Kumiliki maana yake kuweka kitu au jambo (kama vile mali na madaraka) ndani ya himaya au udhibiti (BAKITA, 2017). Hivyo, umilikishwaji wa ardhi ni hali ya mtu au kundi la watu kupewa ardhi na kuiweka katika himaya yao na kuidhibiti. Umilikishwaji wa ardhi hufanywa kwa njia halali au hata zisizo halali (ambazo huhalalishwa hata kilazima). Hivyo, wakati mwingine, kwa muktadha wa utandawazi, umilikishwaji wa ardhi huambatana na tendo la kudhulumu haki ya kumiliki ardhi kwa wananchi wa kawaida na kuikabidhi kwa wageni kutoka nje ya nchi na viongozi wachache. Aidha, Mohamed (2010) anasema kuwa, wageni kutoka nchi za Magharibi, hususani Wazungu, Waarabu na Waasia, huja katika nchi zinazoendelea, hasa Bara la Afrika, kwa malengo yao binafsi, ikiwamo kumiliki ardhi kubwa kwa maendeleo yao. Watu huporwa au kuondolewa katika maeneo yao kwa kisingizio cha

uwekezaji. Maelezo haya yanaungwa mkono na Shivji (2006) anaposema kuwa maelfu ya hekari za ardhi katika Masai, Barabaig na Mbulu zimechukuliwa na kuporwa na wawekezaji na kuwaacha wakazi wa maeneo hayo wakikosa maeneo ya makazi, malisho ya mifugo yao na maeneo ya kulima. Hata hivyo, umilikishwaji wa ardhi si dhana ngeni, ilikuwepo kwenye jamii zetu tangu zamani, hata kabla ya utandawazi kuenea. Hoja hii inaungwa mkono na Boone (2014) anayesema kuwa, kabla ya utandawazi, umilikishwaji wa ardhi uliendeshwa zaidi na misingi ya kitamaduni (kama vile mila, desturi, mahusiano ya kijamii na mamlaka ya jadi). Baada ya sheria zilizoandikwa kuingizwa katika mifumo ya kisasa ya kisheria, utandawazi na ukoloni vilibadilisha mifumo hii kwa kuanzisha umilikishwaji binafsi na hatimiliki za kisheria. Hapo ndipo wawekezaji kutoka nchi za nje walipoingia nchi za Afrika na kufanya umilikishwaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Hivyo, umilikishwaji wa ardhi umechukua sura mpya inayoendana na mabadiliko ya maendeleo ya wakati wa utandawazi tulionao sasa.

Riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) imesawiri suala la umilikishwaji wa ardhi kwa kumtumia mhusika Delpiero aliyemiliki ardhi kubwa kwa maendeleo yake binafsi, na kuacha wenyeji wakihangaika hata kukosa kumiliki ardhi ndogo kwa maendeleo yao na nchi kwa ujumla. Mwandishi anasema:

> **Data Na. 4**
> Inasemekana Delpiero karibuni amemeza eneo zima la ardhi la pahala fulani tumboni mwake. Wavuvi waliposimama kidete kupuliza cheche zao za uchungu, K alikuja juu kuwaambia wastarehee neema zao. Kisha alivuta hewa mapafuni mwake kuzizima cheche zenyewe kwa pumzi zote alizoweza kuzitoa. Nini kwa hakika Delpiero anafanya hasa haikujulikana, ila wavuvi waliomwona wanahadithia kwamba walimshuhudia mara kadha akiota mbawa na kuruka, akitokomea pahala fulani,

> kisha kurudi na kudondosha magunia yaliyojaa unga (uk. 13).

Nukuu hiyo inaonesha umilishwaji ardhi usio wa kihalali, pale ambapo Delpiero alivyojimilikisha eneo kubwa la ardhi kwa ajili ya shughuli zake binafsi, huku watu wengine wakiwa na uhaba wa maeneo. Lengo la kujimilikisha ardhi hiyo ni kujilimbikizia mali. Suala hili, kama isemavyo Nadharia ya Uhalisia, kupitia mhimili unaosisitiza kuwa sanaa iwakilishe ukweli kwa maneno halisi, inaendana na hali halisi ya mazingira ya sasa ya umilikishwaji ardhi usio halali. Kiuhalisi, wawekezaji na watu wenye uwezo wa kifedha kama Delpiero hujimilikishia ardhi kubwa kwa njia zisizo halali (Mohamed, 2001). Jambo hilo hufanya wananchi kusononeka wanapodhulumiwa ardhi yao, na pengine kukosa maeneo ya kuendeshea shughuli zao za kila siku.

Vilevile, wageni toka nchi za Magharibi walikuja Afrika wakiwa na malengo ya kuchunguza ardhi na kujua kama ina madini mbalimbali au la. Haya yanadhihirika kupitia data ifuatayo:

> **Data Na. 5**
> Mbali na hayo, waliowahi kuwa karibu na Miyazawa wanasema kafuga kucha zenye urefu wa meli nzima, na hupita maeneo mbalimbali kunukiliza harufu fulani kama mbwa. Baadaye akigundua kitu, huanza kuchimba kwa kucha zake mwaka mzima mfululizo. Na kila mwenyeji anayepita na kumwona humwuliza, “Unachimba nini?” Na yeye hujibu, “Dhahabu na almasi…” Wenyeji bila ya shaka hucheka na kuridhika na upumbavu wake (uk. 14).

Dondoo hili linaonesha jinsi wageni kutoka nje walivyomiliki maeneo makubwa ya ardhi, na jinsi walivyoyatawala mpaka kufanya uchimbaji wa madini. Miyazawa anayetajwa katika nukuu hii alitembelea maeneo mbalimbali ili kubaini penye madini. Alichunguza ardhi kwa kuchota udongo

na ukucha wake na kugundua iwapo ardhi ina dhahabu au almasi. Baada ya kugundua kama udongo una madini, alijimilikisha ardhi na kupata dhahabu au almasi kwa manufaa yake. Nadharia ya Uhalisia, kupitia mhimili unaosisitiza kuwa sanaa iendane na mabadiliko ya maudhui ndani ya jamii husika, inathibitisha hali halisi ya maudhui haya. Hii ni kwa sababu, katika jamii ya nchi nyingi zinazoendelea, kuna wimbi la umiliki wa ardhi kwa njia zisizo za halali kwa wageni kutoka nje na matajiri wachache kwa maslahi yao binafsi (Mohamed, 2001). Kwa ujumla, riwaya hii inaifikishia jamii ujumbe kwamba umiliki wa ardhi, hasa kwa wageni kutoka nje, unawafaidisha wao kwa kiasi kikubwa na kuacha wananchi wakitaabika hata kukosa eneo dogo kwa ajili ya maendeleo yao.

Halikadhalika, riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* (2002) imesawiri suala la umilikishwaji wa ardhi usio wa halali kwa namna mbalimbali. Inatuonesha kuwa viongozi na wageni kutoka nchi za Magharibi wanajimilikisha maeneo makubwa ya ardhi kwa njia zisizo za halali. Mfano wa viongozi hao ni Luhala ambaye ni mbunge aliyejimilikisha eneo kubwa katika Kijiji cha Ruhimba kwa kuongopa kwamba serikali inataka eneo hilo ili ijenge kiwanda cha mafuta ya alizeti. Mwandishi anasema:

> **Data Na. 6**
> Tuliamini kwamba itakuwa ni rahisi kwake kuelewa kwa sababu hata yeye, mheshimiwa Mbunge, alikuwa anamiliki mapori pale kijijini. Kwa hiyo sisi tulijiona kama watu wake kabisa kuliko wengine wa vijiji vingine katika jimbo letu. Lakini hayo siyo niliyoyakuta Dodoma (uk. 42).

Kupitia nukuu hii, tunaona jinsi umilikishwaji ardhi usio halali ulivyojitokeza kwa Mbunge Luhala pale anapomiliki mapori kijijini. Watu wenye nafasi ya kujimilikisha ardhi kubwa kwa njia zisizo halali ni viongozi wenye nyadhifa

mbalimbali na wageni kutoka nje ya nchi, huku wananchi wa kawaida wakiwa na uhaba wa kumiliki ardhi kwa ajili ya shughuli zao za kila siku.

**Kushamiri kwa ubinafsishaji**

Ubinafsishwaji ni mchakato wa kuhamisha umiliki, udhibiti au uendeshaji wa mali, huduma au shirika kutoka serikalini kwenda sekta binafsi (Wangwe na wenzake, 2014; TUKI, 2019). Selemani (2012) anaongeza kuwa ubinafsishaji hufanywa na watu ili kujipatia kipato binafsi na kusahau watu wengine kulingana na mahitaji yao muhimu. Anaongeza kuwa, katika miaka ya hivi karibuni, nchi nyingi za Afrika zimeingia katika sera ya ubinafsishaji na uwekezaji, hivyo kusababisha wageni kutoka nje kuingia kwa kasi kuja kufanya ubinafsishaji katika maeneo mbalimbali. Kwa upande mwingine, Mwakikagile (2002) anasema kuwa ubinafsishaji ulikuwepo tangu zamani, ingawa kwa kiwango kidogo na, mara nyingi, katika muktadha wa ndani ya nchi. Kwa mfano, baadhi ya mali za kijamii kama vile mashamba, misitu au migodi ilipewa watu binafsi au familia zilizokuwa na mamlaka. Vilevile, ubinafsishaji ulijitokeza katika baadhi ya huduma kama vile maduka, shule au hospitali. Ubinafsishaji huu ulifanywa na kundi au jamii, na ndio maana kulikuwa na shule za wakulima au maduka ya ushirika yaliyosimamiwa na jamii ili kutoa huduma kwa jamii.

Kutokana na kuingia kwa utandawazi, ubinafsishaji umechukua sura mpya. Hii ni kutokana na kwamba jamii huingiliana na kupata mabadiliko kulingana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Aidha, Ubinafsishaji unahusisha kujilimbikizia mali na kutowajali watu wengine. Kwa ujumla, katika muktadha wa utandawazi, ubinafsishaji hudhihirika pale ambapo viongozi pamoja na watu wenye uwezo kiuchumi hujali nafsi zao kwa

kujimilikisha mali za umma bila kujali watu masikini au wale wanaowaongoza. Tulibaini kuwa riwaya teule zimesawiri suala hili.

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, wizi kupitia ubinafsishaji umesawiriwa na akina Di Livio, Miyazawa, Von Heim, Delpiero pamoja na K. Wahusika hawa walifanya wizi kupitia ubinafsishaji kwa kumiliki ardhi kubwa na kuanzisha ujenzi wa Neo-Casino (ukumbi wa kifahari). Mwandishi anasema:

> **Data Na. 7**
> Jengo la Neo-Casino lilisimama kwa fahari ilioje! Lilikuwa jinamizi la kigeni. Limekwenda juu kuliko kitu chochote pale jijini. Kutoka juu likatazama chini kwa dharau kila hatua, kila mtu, kila kitu na kujitangazia ushindi hatimaye (uk. 28).
>
> Na fahari ya Neo-Casino inakamilishwa ndani si nje. Mavyumba yake ya kujimwaya, kwa wakati huu yamekogeshwa anga la umeme. Na nje limevishwa mikufu ya mataa ya rangi na kunywishizika mbalamwezi. Na bustani zake zinazochekelea mchana na usiku na mifereji yake isiyositisha tamasha la kurusha na kumimina maji ingawa maji adimu kokote kwengine (uk. 29).

Katika nukuu hii ubinafsishaji umeonekana katika ardhi iliyojengwa jengo la Neo-Casino, ambalo limetumia fedha nyingi za serikali na nyingine kutoka kwa akina Di Livio, Miyazawa na Delpiero. Neo-Casino ilijengwa kwa ajili ya starehe. Wakati wananchi wa kawaida wanakosa huduma muhimu kama vile maji, mifereji ya Neo-Casino ilikuwa ikitiririsha maji na kuyamwaga kila upande. Viongozi na wageni kutoka nje hawakuwa na dhiki, kwa kuwa mahitaji muhimu yote waliyapata kirahisi. Ubinafsishaji umefungua milango kwa wawekezaji wa kigeni kununua na kuwekeza ardhi ya serikali, hali ambayo imesababisha kuimarika kwa utandawazi. Hata hivyo, serikali imeamua kuuza na kukabidhi ardhi kwa wawekezaji

binafsi kutokana na shinikizo la utandawazi linalotaka uchumi uendeshwe na sekta binafsi (Wangwe na wenzake, 2014). Kwa upande mwingine, Ntarangwi (2004) anasema kuwa, katika hali halisi, sanaa hubadilika kutokana na mabadiliko ya jamii husika. Hii inathibitika kwa ubinafsishaji katika zama za utandawazi kujitokeza katika sura mpya kutokana na mabadiliko ya jamii ya sasa.

Halikadhalika, riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* imesawiri suala la wizi kupitia ubinafsishaji kwa kuwatumia viongozi na wageni kutoka nje wanaomiliki vitu mbalimbali vinavyowanufaisha wao. Mwandishi amemtumia Bwana Pierre Louis, Mfaransa, ambaye, kupitia ubinafsishaji, anajilimbikizia mali kwa kumiliki makampuni matano ya uwindaji huko Dar es Salaam, ikiwamo Golden Hunting Safaris, kama inavyoonekana katika data Na. 8.

> **Data Na. 8**
> Huko alikutana na watalii wa Kimarekani ambao walimtambulisha kwa kamanda wa jeshi mstaafu ambaye aliutumia muda wake kwa kuwaongoza watalii wawindaji wa kampuni ya Golden Hunting Safaris iliyomilikiwa na bwana Pierre Louis (uk. 20-21).

Dondoo hili linaonesha ubinafsishaji pale ambapo bwana Pierre Louis anamiliki kampuni ya uwindaji ambayo inampa faida kubwa. Wangwe na wenzake (2014) wanaunga mkono fikra hii kwa kusema kuwa umiliki binafsi unaweza kuongeza uzalishaji kwa sababu ardhi inasimamiwa kwa uangalifu zaidi na kwa kuzingatia faida ya mmiliki.

Kupitia msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaosisitiza sanaa iwe na uhalisi ambao hubadilika kutokana na mabadiliko ya jamii husika, tulibaini kuwa mwandishi amefanikiwa kuonesha maisha halisi ya jamii kwa kumtumia

mhusika Pierre Louis aliyefanya ubinafsishaji katika makampuni na viwanda. Hali hii inaakisi uhalisi, ambapo katika jamii nyingi za nchi zinazoendelea kuna watu wenye nyadhifa ambao hufanya ubinafsishaji kwa kudhulumu ardhi, mali na pengine nguvu kazi kutoka kwa wananchi wa kawaida.

Vilevile, Paul Mooney anamshauri Jonathan Masawe kugombea ubunge akiwa na matumaini kwamba akipata atawasaidia na kuwatetea wafanyabiashara na wawekezaji, watakapohitaji ardhi kwa ajili ya kujibinafsisha. Wageni kutoka nje ya nchi waliamini hivyo kwa sababu Jonathan Massawe alikuwa anajipendekeza kwao na kuwasaliti wananchi wenzake. Mwandishi anasema:

> **Data Na. 9**
> Jonathan Masawe alianguka vibaya sana katika jaribio lake la kutaka kugombea ubunge kwa ushauri wa Paul Mooney, ambaye alidhani kwamba kama angepata ubunge, labda angeweza kupata hata uwaziri, jambo ambalo lingekuwa la manufaa sana, hususani kwa wafanyabiashara na wawekezaji (uk. 92).

Nukuu hii inaonesha jinsi wageni kutoka nje ya nchi walivyokuwa na ubinafsi na ulafi. Kupitia msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaosisitiza kuwa sanaa lazima ioneshe hali halisi ya matukio katika jamii husika, tulibaini kuwa mwandishi amefanikiwa kuonesha maisha halisi ya jamii kwa kumtumia mhusika Paul Mooney ambaye anawakilisha viongozi wenye tamaa na ulafi ambao unaowafanya wajilimbikizie mali, huku wakiwaacha wananchi wakiwa na hali ngumu ya kimaisha.

**Kuingizwa kwa utamaduni wa kigeni**

Utamaduni wa kigeni ni mfumo wa maisha, fikra, lugha, imani, maadili na mbinu za jamii nyingine, unaoingizwa katika jamii kwa njia ya ukoloni, elimu, dini au utawala na ambao mara nyingi hubadili utamaduni wa asili wa jamii husika (Thiong'o, 1967). Selasi (2010) anaongeza kuwa utamaduni wa kigeni huwa na vipengele kama vile mila na desturi, mavazi, chakula, na lugha ambavyo mtu hakukulia ndani yake. Kwa ujumla, utamaduni wa kigeni ni ile hali ya kuiga au kupokea mila na desturi za kigeni kutoka kwa wageni, yaani watu kutoka na kadhalika. Wageni kutoka katika mabara kama vile Ulaya, Asia, Uarabuni wanapoingia nchi za Afrika huja na utamaduni wao mpya ambao watu huuiga na kuufuata. Katika hali halisi, kabla ya kuingia kwa utamaduni wa kigeni, Waafrika walikuwa na utamaduni wao. Utamaduni huu wa asili umepata mabadiliko kutokana na baadhi ya Waafrika kutaka wafanane na Wazungu. Hali hii imesababishwa na jamii kukua, kuendelea na kupokea mabadiliko kwa kuiga utamaduni wa kigeni. Riwaya zilizotafitiwa zimesawiri hali hii kama inavyojadiliwa katika aya zinazofuata.

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, mwandishi ameonesha jinsi utamaduni wa kigeni unavyoikumba jamii ya sasa. Utamaduni wa kigeni unahusisha mambo mengi yaliyoletwa na wageni katika jamii yenye asili nyingine. Miongoni mwa mambo hayo ni nywele, rangi ya ngozi, nguo na kucha. Mtu anapotaka kuendana na utamaduni wa kigeni ni lazima anunue vifaa vitakavyomfanya awe kama Mzungu. Thiong'o (1967) anasema kuwa fikra za Waafrika wengi ni kwamba mitindo ya maisha ya Kimagharibi ni bora kuliko ya Kiafrika, hali hii inasababisha baadhi ya Waafrika kuiga mambo ya kigeni, kama kuchubua ngozi ili iwe nyeupe au kutumia nywele bandia ili kuthibitisha wako sawa na Wazungu. Hali hii inadhihirisha kuwa Waafrika hatupendi asili yetu. Mwandishi amedhihirisha haya kwa kusema:

**Data Na. 10**

> Mnarejeshwa nyuma kwenye ule uliokuwa ukiiitwa ushenzi, kwa kile kinachoitwa usasa na fesheni. Na ubaya wa mambo hayo yote mnayanunua kwa bei rahasi na kwa sababu mifuko yenu mitupu, tayari kufanya dhambi yoyote ile kuigundua fedha ya kununulia. Ah, tunapofikia hadi kuona rangi zetu si bora tena, nywele zetu hazifai kamwe, pua zetu… midomo yetu… sijui kiasi gani cha ubinadamu wetu kinabaki? (uk. 51)

Nukuu hii inaonesha jinsi utamaduni wa kigeni ulivyojitokeza katika jamii za Kiafrika. Waafrika wengi hudharau utamaduni wao na kufuata wa kigeni ili wawe wa kisasa. Kupitia msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaosisitiza kuwa sanaa iwe na uhalisi ambao hubadilika kutokana na mabadiliko ya jamii husika, tulibaini kuwa mwandishi amefanikiwa kuonesha maisha halisi ya jamii kwa kuwatumia wahusika wasichana waliochubua rangi za ngozi zao. Walifikia hatua ya kuona kwamba rangi zetu si bora, nywele zetu hazifai kamwe, pua na midomo yetu haifai, bali mwonekano unaofaa ni ule wa Kizungu. Hivyo, waliweka nywele bandia na kope bandia. Kufanya hivyo ni kuiga utamaduni wa kigeni unaoenda sambamba na utandawazi na unaoonekana ni bora kuliko ule wa asili (Thiong'o, 2009)

Kwa upande mwingine, utamaduni wa kigeni umejitokeza katika kipengele cha mavazi. Mavazi yasiyositiri vizuri miili yetu yameingia katika nchi za Afrika kipindi cha utandawazi. Baadhi ya mavazi hayo ni kama vile sketi fupi na fulana fupi zinazoachana sehemu ya tumbo ikiwa wazi. Isaiah (2025) anaongeza kuwa maadili katika mavazi yamebadilika kupitia mitandao ya kijamii kama vile *Instagram*, *TikTok* na *YouTube*. Vijana wengi wanaiga mitindo ya Kimagharibi inayosisitiza kuonesha maungo ya mwili. Hali hii imepunguza thamani ya mavazi yaliyokuwapo

katika jamii zetu za Kiafrika zinazotilia mkazo heshima na ustaarabu. Mwandishi anasema:

> **Data Na. 11**
> Wale wanawake waliokuwa vimada; baadhi sura zao alizitambua. Aligeuza uso kutowatizama, ingawa alijua wao hawamuoni. Wote wamevaa mini (sketi fupi) na vitopu (fulana fupi) na viatu vya mabloki, virefu mno hata vimewafanya waonekane makomanzi. Midomo inameremeta wekundu useme mafirigisi mabichi (uk. 27 – ufafanuzi wa kwenye mabano ni waandishi wa makala hii).

Dondoo hili linaonesha jinsi ambavyo Waafrika wameuacha utamaduni wao na kufuata utamaduni wa kigeni ulioshamiri zama za utandawazi. Wanawake wameoneshwa wakiwa wamevaa mini sketi na vitopu, huku baadhi ya maungo ya miili yao yakiwa wazi. Kupitia msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaosisitiza kuwa sanaa lazima ioneshe hali halisi ya matukio katika jamii husika, tulibaini kuwa mwandishi amefanikiwa kuonesha maisha halisi ya jamii kwa kuwatumia wahusika wanawake. Hii ni kwa sababu baadhi ya wanawake katika jamii za Kiafrika huvaa nguo fupi kwa kuiga mwonekano wa Kizungu. Vilevile, mwandishi anatoa ujumbe kwa jamii kuwa tupende asili yetu, tusiige utamaduni wa kigeni ambao ni tofauti na maadili ya utamaduni wetu.

Kwa upande wa riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria*, mwandishi amesawiri suala la utamaduni wa kigeni kupitia wahusika wachezamuziki pamoja na vijana waliokuwa wanafanya vitendo vilivyo nje ya utamaduni wa Kiafrika. Mwandishi anasema:

> **Data Na. 12**
> Bendi ya muziki ilikuwepo, ikipiga nyimbo za kuigiza za kutoka nje… Wasichana watatu waliokuwa pale mbele, wakiwa wamevaa nguo ambazo zilisitiri matiti na sehemu ndogo tu za maungo ya uzazi; walikuwa wakicheza. Nao

> walishangiliwa kwa nguvu sana kadiri walivyochezesha nyonga zao na kubinua viuno vyao kwa ufundi ulioashiria vitendo vya ngono… Wengine walikuwa wakipigana mabusu, na baadhi walikuwa wakitoka pale na kuvutana hadi nyumbani, au nyuma ya miti kwenda kukidhi mioto ya ashki ya miili yao (uk. 84).

Nukuu hii inaonesha wasichana wakicheza huku wakiwa wamevaa nguo zilizositiri baadhi tu ya sehemu zao za siri. Vilevile, inaonesha vijana wakivutana pembeni ya miti kwenda kukidhi haja za miili yao. Kupitia msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaosisitiza kuwa sanaa lazima ioneshe hali halisi ya matukio katika jamii husika, tulibaini kuwa mwandishi amefanikiwa kuonesha maisha halisi ya jamii. Hii ni kwa sababu, katika jamii yetu, kuna wasichana na wanawake ambao huona fahari kufuata utamaduni wa kigeni. Kwa upande mwingine, mwandishi anatoa funzo kwa jamii kuwa yatupasa tuthamini utamaduni wetu.

**Ukwepaji wa kodi**

Ukwepaji wa kodi ni kitendo cha kutolipa kodi kwa kutumia mianya inayoruhusiwa na sheria (Kalegeya, 2012). Selemani (2012) anaongeza kuwa ukwepaji wa kodi hufanyika kwa mtu binafsi au kampuni kupanga shughuli kwa njia inayopunguza kiwango cha kodi kinachotakiwa kulipwa, lakini bila kuvunja sheria. Kwa ujumla, ukwepaji wa kodi hutokea pale ambapo watu binafsi, shirika, kampuni au taasisi husaka mianya ya kutolipia kodi. Kalegeya (ktj) anasisitiza kuwa ukwepaji wa kulipa kodi unaofanywa na makampuni mbalimbali ya biashara na wafanyabiashara ni tatizo linaloisumbua Mamlaka ya Mapato Tanzania. Pia, huikosesha nchi mapato ambayo yangetengwa kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma bora za kielimu, afya, maji na miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Kwa mujibu

wa Wangwe na wenzake (2014), suala la ulipaji kodi linasumbua sana wafanyabiashara na makampuni mbalimbali kutokana na kiwango cha kodi kuwa kikubwa. Hali hii, hatimaye, husababisha kukwepa kulipa kodi kwa kutumia mbinu mbalimbali. Hata hivyo, suala la ukwepaji kodi si geni, lilijitokeza hata katika jamii na tawala za kijadi kupitia ufichaji wa mazao katika jamii za wakulima, ingawa kwa sasa limepokea mabadiliko. Mabadiliko hayo yamesababishwa na utandawazi ambao umeongeza fursa za watu na makampuni kufanya biashara huru za kimataifa. Jambo hilo linaweza kurahisisha kukwepa kulipa kodi ikiwa hakuna usimamizi makini. Waandishi wa riwaya zilizotafitiwa wamedhihirisha suala hili kama inavyojadiliwa katika aya zinazofuata.

Katika riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria*, ukwepaji kodi umedhihirika pale mwandishi anapoelezea jinsi mashirika na makampuni binafsi yanapokwepa kulipa kodi na kuingiza bidhaa kwa njia ya magendo na wakati mwingine kutoa hongo (Chachage, 2002). Ukwepaji kodi hurudisha nyuma maendeleo ya nchi kwa vile kodi husaidia kuendeleza mambo mbalimbali. Mwandishi wa riwaya hii teule anaonesha kuwa wanahabari kama vile Mjuba na Sifuni hawakupenda suala hili la ukwepaji kodi kuendelea kufanyika, hivyo walijifunga kibwebwe kufichua uovu huo. Katika ufichuaji huo, Mjuba na Sifuni wanatekwa. Mwandishi anasema:

> **Data Na. 13**
> Ilikuwa kesi iliyomhusu Mjuba na Sifuni. Habari zilikuwa zimeenea mjini kote. Mjuba na Sifuni walikuwa wametekwa nyara na majambazi matatu siku chache zilizopita. Hayo majambazi yalitaka kujua kama Mjuba alikuwa amezipata wapi habari za ukwepaji wa kodi wa baadhi ya mashirika ya uingizaji wa bidhaa (uk. 6).

> Ilikuwa ni wazi kwamba hawa watuhumiwa walikuwa wametumwa na hao wakwepa kodi, kwani mambo ya waandishi wa habari kutishiwa kwa kufichua madhambi yalikuwa yameshaanza kuwa ya kawaida nchini (uk. 8).

Nukuu hii inaonesha jinsi ukwepaji kodi kama kipengele cha utandawazi kilivyojitokeza katika riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria*. Wageni kutoka nje walikwepa kulipa kodi ili kuongeza faida yao inayopatikana kutoka katika miradi waliyoianzisha na bidhaa wanazoingiza nchini. Kupitia msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaosema kuwa sanaa iwe na uhalisi ambao hubadilika kutokana na mabadiliko ya jamii husika, tulibaini kuwa mwandishi amefanikiwa kuonesha maisha halisi ya jamii. Hii kwa sababu katika maisha halisi kuna wafanyabiashara ambao hukwepa kulipa kodi ili wapate faida zaidi.

Vilevile, ukwepaji kodi umedhihirika kupitia Bwana Chaurembo anayehusika na uingizaji na utoaji wa bidhaa za Bwana Alibhai kupitia shirika lao bila kulipia kodi kama inavyodhihirika katika data Na. 14.

> **Data Na. 14**
> Alibhai aliposikia kwamba Chaurembo alikuwa akidai shilingi milioni tatu zaidi alikasirika sana, kwani, kwa kawaida, alizoea kumpa milioni moja au mbili kila wakati aliposaidia kuingiza au kutoa bidhaa zake kupitia shirika lao bila ya kulipa kodi (uk. 181).

Nukuu hii inaonesha jinsi Alibhai na wafanyabiashara wenzake walivyokuwa wanakwepa kulipa kodi na badala yake walitoa hongo ili waingize na kutoa bidhaa zao. Kupitia msingi unaosema kuwa sanaa iwe na uhalisi, tulibaini kuwa mwandishi amefanikiwa kuonesha maisha halisi ya jamii. Hii ni kwa sababu, katika nchi nyingi zinazoendelea kuna malalamiko kuhusu baadhi ya wafanyabiashara wakubwa ambao hujihusisha na magendo na ukwepaji kodi. Kwa kufanya hivyo,

huikosesha nchi mapato kupitia kodi. Mwandishi anatoa ujumbe kwa jamii kuwa maendeleo ya nchi huambatana na mapato mbalimbali ya serikali kama vile kulipa kodi, hivyo anashauri kodi ilipwe kwa maendeleo ya nchi.

## Hitimisho na Mapendekezo

Makala hii imejadili ujitokezaji wa vipengele vya utandawazi katika riwaya za kisasa za Kiswahili. Matokeo ya makala hii yamebainisha vipengele vitano vya utandawazi vilivyojitokeza katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili. Vipengele vya utandawazi vilivyobainishwa ni pamoja na kushamiri kwa uwekezaji, umilikishwaji wa ardhi, kushamiri kwa ubinafsishaji, kuingizwa kwa utamaduni wa kigeni, na ukwepaji wa kodi. Aidha, matokeo ya utafiti yamedhihirisha kuwa vipengele vya utandawazi hujitokeza katika riwaya za kisasa za Kiswahili kutokana na ukweli kwamba waandishi huakisi mabadiliko yanayoendana na wakati husika. Makala hii inapendekeza tafiti zifanyike kuhusu ulinganisho wa fani au maudhui baina ya riwaya za kisasa za Kiswahili na riwaya za Kiswahili zilizoandikwa kabla ya utandawazi. Hii itasaidia kwa wanafasihi kuweza kujua namna fani na maudhui vinavyobadilika kulingana na wakati husika.

## Marejeleo

BAKITA. (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Ltd.

Boone, C. (2014). *Property and Political Order in Africa: Land Rights and the Structure of Politics*. Cambridge: Cambridge University Press

Chachage, C. L. (2002). *Makuadi wa Soko Huria*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Dunning, J. H. (1992). *Multinational Enterprises and the Global Economy*. Reading, MA: Addison-Wesley.

Hegel, G. W. F. (1971). *Introduction to Aesthetics*. Oxford: Clarendon

Isaiah, O. M. (2025). Religious atonement as a response to indecent dressing among christian youths. *International Journal of Religious, Culture and Peacebuilding,* 10(2) 23-28.

Jean, T. (2002). *The Hidden Dimension of Globalization. What is at stake geoculturally? Global Policy Forum.* New York: ATTAC.

Kalegeya, T. (2012). *Riwaya ya Kiswahili na Utandawazi: Uchunguzi wa Makuadi wa Soko Huria na Almasi za Bandia* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Kevogo, A. U. (2017). Taswira ya Utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya *Dunia Yao*. Katika *Kioo cha Lugha*, 15, 31-49.

Kezilahabi, E. (2006). Utandawazi, Kiswahili na Dhana ya Wakati. Katika S. Sewangi na J. Madumulla (wah) *Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI-2005: Kuadhimisha Miaka 75 ya Uchunguzi wa Kiswahili (1930-2005).* (kur. 164-172). Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

Lukacs, G. (1979). *The Meaning of Contemporary Realism*. London: Merlin

Masimo, D. B. (2023). *Mkengeuko wa Utamaduni wa Waswahili katika Riwaya ya Kiswahili zama za Utandawazi* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, S. A. (2010). *Muswada wa Riwaya na Makala Mbalimbali kuhusu Fasihi na Utandawazi*. Zanzibar: Dira.

Msokile, M. (1993). *Miongozo ya Lugha na Fasihi: Uchambuzi na Uhakiki wa Riwaya.* Dar es Salaam: TUKI

Musembi, N. na Simiyu, F. (2024). Usawiri wa Vijana wa Kisasa katika Riwaya ya *Dunia Yao* ya Kiswahili. *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili,* 7(1), 1-10.

Mwakikagile, G. (2002). *Nyerere and Africa: End of an Era*. Dar es Salaam: Mkuki wa Nyota.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi* (Ph.D Thesis, Unpublished). Augustana College, Rock Island.

Nyonje, J. W. (2006). *Mwono Ulimwengu wa Waswahili*. Nairobi: University of Nairobi Press.

Oni, A. A. (2005). Globalization and Its Implications on Africa Culture and Development: Challenges for Education. *International Journal of African and African American Studies,* 4(2), 86-105.

Selasi, T. (2010). *Don't Ask Where I'm From, Ask Where I'm a Local [Essay].* Imepakuliwa kutoka: https://www.brainpickings.org/2025/10/11. 12.10.

Selemani, L. O. (2012). *Riwaya Mpya ya Kiswahili na Masuluhisho ya Changamoto za Utandawazi* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Senkoro, F. E. M. K (2007). Uhalisiamazingaombwe katika Fasihi ya Kiswahili: Istilahi Mpya, Mtindo Mkongwe. *Jarida la Kiswahili la Isimu na Fasihi*, 3(21), 78-101.

Shivji, I. G. (2006). *Let the People Speak, Tanzania Down the Road to Neo-Liberalism*. Senegal: Codersia.

Suakei, S. (2017). *Utamaduni na Utandawazi*. Kenya: University of Nairobi Publishers.

Thiong'o, N. (1967). *A Grain of Wheat*. New Hampshire: Heinemann.

Thiong'o, N. (2009). *Something Torn and New: An African Renaissance*. New York: Basic Civitas Books.

Thomas, L. F. (2005). *The World is Flat*. New York: Picador

TUKI (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press East Africa Limited.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.

Wangwe, S., Mmari, D., Aikaeli, j., Rutatina, N., Mboghoina, T., na Kinyondo, A. (2014). *The Performance of the Manufacturing Sector in Tanzania*. Dar es Salaam: UNU-WIDER.